



Maswali

1. Abramam aliishi kwa mji gani?
2. Mungu alitaka Abramam afanye nini?
3. Abramam alimpenda Mungu na kumtii?
4. Nani alienda na Abramam kutoka mji wa Uru?
5. Walikaa kwa mji gani mpaka babake Abramam akafa?
6. Abramam alijua namna gani mji wenye Mungu alitaka aende?
7. Jina la nchi hiyo iliitwaje?
8. Abramam alifanya nini alipofika kwa hiyo nchi?
9. Ahadi 3 gani zenye Mungu aliahidi Abramam?
10. Hizi ahadi zimekamiliika namna gani?

Majibu

1. Uru
2. Kuondoka Uru na aende kwa nchi atakayomwonyesha.
3. Ndiyo.
4. Babake Abramam, mkewe –Sarai na mpwake –Lutu.
5. Harani.
6. Mungu alimwonyesha njia ya kuendea.
7. Kanaani.
8. Alijenga madhabahu na kutolea Mungu sadaka ya shukrani.
9. 1. Atakuwa na wazao wengi –taifa kubwa.
2. Atakuwa na umaarufu.
3. Atakuwa na mzao wa kipekee naye atafurahisha kila mtu.
10. 1. Taifa la Wayahudi ndio uzao wa Abramam.
2. Mpaka sasa bado tunasoma juu ya Abramam – kwa hivyo ana umaarufu.
3. Yesu atafuraisha kila mtu katika Ufalme.

4 Mwito wa Abramam

Kwa Biblia Mwanzo 12:1-4; Waebrania 11:8-10


Kiini cha somo

Kuonyesha vile Abramam alipewa ahadi kuu na Mungu. Abramam aliamini na kumtii Mungu.

Somo

Karibu na mto wa Frati kulikuwa mji ulioitwa Uru. Uru ulikuwa mmoja ya miji mikuu kwa hiyo nchi. Ikulu ya mfalme ilikuwa Uru. Watu wa Uru hawakuabudu Mungu wa kweli. Waliabudu mwezi. Katikati ya Uru kulikuwa hekalu kubwa ya mungu wao mwezi.

Mji wa Uru



Kulikuwa na shughuli nyingi Uru. Tena palikuwa mahali pazuri pa kuishi. Kulikuwa na uwanja na bustani nzuri. Kulikuwa na maktaba, maduka na shule. Watu wa Uru walikuwa matajiri na walikaa kwa nyumba kubwa.

Mtu aliyeitwa Abramam pamoja na familia yake waliishi Uru. Walikuwa tajiri na waliishi kwa nyumba kubwa. Walikuwa na watumishi wengi. Watu wa Uru waliabudu mwezi – mungu asiye wa kweli. Lakini Abramam alimpenda Mungu wa kweli na alimwabudu.

Siku moja Mungu alimwambia Abramam, “Nataka utoke kwa mji huu. Ondoka nyumbani kwenu uwache familia na marafiki yako. Itakulazimu usafiri mwendo mrefu uende nchi ya mbali. Nitakuonyesha njia ya kuendea. Ukinitii nitakubariki.”

Mungu alitaka kujua kama Abramam atampenda zaidi ya utajiri wake, jamii yake na hata marafiki wake. Mungu alitaka kuona kama kweli Abramam atamwamini atoke nyumbani kwao na aende vile Mungu alitaka.


Mungu alimchagua Abramam kutoka kwa maelfu ya uzao wa Nuhu. Mungu alimchagua kwa sababu alikuwa mwaminifu na wa haki. Mungu alimchagua awe baba wa watu waliowakipekee wa Mungu. Mungu alimpa Abramam ahadi sizizo za kawaida.

Abramam alipenda Mungu sana. Alifanya alichambiwa na Mungu. Abramam aliondoka mji wa Uru na baba yake, mkewe Sarai na mpwa wake Lutu. Aliondoka mji wa Uru na akaenda upande wa kaskazini.

Abramam alipenda Mungu sana. Alitii Mungu. Aliacha nchi yake nzuri sana na marafiki wake wote. Alisafiri mwendo mrefu mno. Alikaa kwa hema na kuishi kwa nchi mgeni penye hakukuwa na marafiki.

Abramam alitaka sana kumfurahisha Mungu ili aishi kwa Ufalme wake. Abramam alitaka hii zaidi ya nyumba yake iliyokuwa nzuri, utajiri wake, jamii yake na hata marafiki. Katika maisha yake alimueka Mungu mbele. Nasi pia tujaribu kumpenda Mungu kuliko kitu chochote. Inatulazimu tumpende Mungu na kumtii tukitaka tukue kwa Ufalme wake.

Kutoka Uru Abramam alienda kaskazini. Babake Abramam alikuwa mzee sana. Alichoka kusafiri kila siku. Abramam alipofika mji wa Harani, alikaa hapo kwa mda na hapo ndipo babake alikufa.



Baada ya baba ya Abramam kufa, Abramam, Sarai na Lutu waliendelea na safari. Mungu aliwaonyesha njia ya kuendea. Mwishowe walifika kwa nchi ya Kanaan. Mungu alitaka wafike kwa hii nchi. Walipofika nchi ya Kanaan, Abramam alitia hema karibu na Betheli. Abramam alijenga madhabahu na akatolea Mungu matoleo ya shukrani. Alimshukuru Mungu kwa kumleta salama kwa nchi mgeni.

Mungu alifurahi kwa sababu Abramam alimpenda na kumtii. Mungu alifurahi kwa sababu Abramam alimwamini na kukubali ahadi zake. Mungu alimbariki Abramam na kumuahidi ahadi tatu sizizo za kawaida.

Ahadi za Mungu kwa Abramam

Abramam atakuwa na wazao wengi. Watakuwa taifa kubwa.
Uzao wa Abramam wamekuwa taifa kubwa. Wayahudi ndiyo hili taifa.

Abramam atakuwa maarufu.

Tunajifunza juu ya Abramam hata sasa, kwa hivyo ako na umaarufu.

Abramam atakuwa na mzao mmoja atakayekuwa wa maana. Huyu mzao wake atafuhisha watu wote ulimwenguni.

Yesu ndio mzao wa Abramam wa maana. Atafurahisha watu wote katika Ufalme.